

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA UKEREWE
MKOA WA MWANZA**

Phone: +255 282 515 056/+255 685 304 646
Email: Ps@ukerewedc.go.tz
Tovuti: www.ukerewedc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P 41,
NANSIO/UKEREWE.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb Na. GA.6/95/01/48

30/03/2021

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA WATENDAJI WA VIJJI DARAJA LA III

Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe kupitia kibali cha ajira mbadala Kumb Na. FA.170/359/01'A/95 kilichotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina Tangaza nafasi wazi mbili (2) za watendaji wa vijiji Daraja la III.

1.0. Sifa za waombaji

Awe amehitimu Elimu ya kidato cha IV au VI na awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/cheti cha Technician Certificate (NTA Level 5) katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo – Dodoma au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

2.0. Kazi za kufanya/majukumu.

- Atakuwa mtendaji na mshauri wa serikali ya kijiji na kamati zake katika mipango ya maendeleo.
- Atakuwa Afisa masuuli na mtendaji mkuu wa serikali ya kijiji na atasimamia mapato na matumizi ya Halmashauri ya kijiji.
- Atakuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika kijiji.
- Atapaswa kuratibu na kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo za Halmashauri ya kijiji.
- Atakuwa katibu wa kamati ya Halmashauri ya kijiji
- Ataongoza vikao vya maendeleo ya kijiji vitakavyohusisha wananchi na wataalam waliopo kwenye eneo lake
- Atapaswa kuhamasisha wananchi katika mikakati mbalimbali ya kuondoa njaa na umasikini katika eneo lake.
- Atakuwa kiongozi wa wataalamu waliopo ngazi ya kijiji.
- Atatekeleza majukumu yote kadri atakavyo kuwa anaelekezwa na mwajiri.

3.0. Ngazi ya Mshahara

Mshahara ni kwa mujibu wa viwango vya mshahara serikalini yaani TGS B1 (390,000/=) kwa mwezi.

4.0. Masharti kwa ujumla

- Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45
- Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa
- Waombaji waambatishe maelezo binafsi (Detail CV) yenye anwani na namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.
- Maombi yote yaambatane na vyeti vya Elimu na Taaluma yaani nakala ya vyeti vya kidato cha Nne au Sita pamoja na vyeti vya Taaluma na picha mbili za rangi za hivi karibuni.
- Testimonial, Provisional results, statement of results, hati ya matokeo ya kidato cha nne (Form IV) na kidato cha sita (Form VI) havitakubalika.
- Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (NECTA na NACTE) na taarifa ya ulinganifu iambatishwe kwenye maombi.
- Waombaji wa nafasi za ajira waliostafishwa, waliofukuzwa kazi na kuachishwa kazi katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
- Barua ya maombi iandikwe kwa mkono tofauti na hapo ombi lako halitapokelewa.
- Kichwa cha habari kitaje nafasi ya kada unayoomba kwa ufasaha
- Barua ya maombi isainiwe na mwombaji mwenyewe tofauti na hivyo maombi husika yatakataliwa.
- Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.


Waombaji watakaokidhi sifa na vigezo watajulishwa tarehe ya ushahidi kwa kupitia namba za simu na anwani walizotumia kwenye barua ya maombi ya kazi.

- Barua zitakazoletwa kwa mkono hazitapokelewa.
- Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **13/04/2021** saa **9:30** alasiri.

Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kupitia anwani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P. 41,
NANSIO/UKEREWE.

Imetolewa na:


Goodluck J. Mtigandi
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
UKEREWE

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
UKEREWE

Nakala: Tangazo hili linapatikana kwenye mbao zote za matangazo za Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, nje ya Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe na kwenye tovuti (webite) ya Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe ambayo ni www.ukerewedc.go.tz.